Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Surua

Je, surua ni nini?

Surua inaambukiza sana na inaweza kusababisha ugonjwa mbaya. Surua husababishwa na virusi na huenea kwa urahisi sana wakati mtu aliyeambukizwa anapumua, anakohoa au anapiga chafya. Ugonjwa wa surua huenea kwa urahisi hivi kwamba mtu yeyote aliye hatarini mwa kuambukizwa na asiye na kinga (iwe kwa kuchanjwa au kuwa na surua hapo awali) anaweza kuambukizwa.

Je, dalili za surua ni gani?

- Homa
- Kamasi kwenye pua
- Kikohozi
- Uvimbe wa mboni ya jicho (wekundu, kutoa machozi)
- Upele kote mwilini

Watu wanaweza kueneza ugonjwa wa surua kabla ya kuwa na dalili. Kwa kawaida dalili hudumu kwa siku 7-10.

Je, ugonjwa wa surua huzuiwa vipi?

Chanjo ya surua, matumbwitumbwi na rubela (MMR) ni salama sana, fanisi na ni kinga bora zaidi dhidi ya surua. Dozi mbili za chanjo ya MMR zinazuia surua kwa ufanisi wa takriban 97%. Dozi moja inazuia ugonjwa huo kwa ufanisi wa takriban 93%.

Kuna milipuko ya surua nchini Marekani na nje ya nchi.

Hivi majuzi watoto wadogo ambao hawajachanjwa wametambuliwa kuwa wana ugonjwa huu jijini Columbus -- visa na mlipuko wa kwanza kuwahi kuripotiwa katika jamii yetu kwa zaidi ya miaka 20. Unaweza kuilinda familia yako kwa chanjo ya surua, matumbwitumbwi na rubela (MMR). Mtu yeyote anayesafiri nje ya nchi, wakiwemo watoto wachanga wenye umri wa miezi 6-11, wanapaswa kuwa wamepata chanjo ya MMR.

Je, surua inatibiwa vipi?

Surua haina tiba. Dawa zinazouzwa bila maagizo ya daktari zinaweza kusaidia kupunguza homa. Kwa kawaida dalili zingine hupungua ndani ya wiki 2-3.

Je, nani anahitaji chanjo ya surua (MMR)?

Watoto - Watoto wanapaswa kupokea dozi mbili za chanjo ya MMR, wakianza na dozi ya kwanza wakiwa na umri wa miezi 12-15 na dozi ya pili wakiwa na umri wa miaka 4-6 au angalau siku 28 baada ya dozi ya kwanza.

Wanafunzi walio katika Taasisi za Elimu ya Baada ya Shule ya Upili - Wanafunzi walio katika taasisi za elimu ya baada ya shule ya upili wasio na kinga dhidi ya surua wanahitaji dozi mbili za chanjo ya MMR na wanahitaji kupata dozi ya pili siku 28 baada ya dozi ya kwanza.

Watu wazima - Watu waliozaliwa wakati au baada ya mwaka wa 1957 ambao hawana kinga dhidi ya surua wanapaswa kupata angalau dozi moja ya chanjo ya MMR.

Wasafiri wa Kimataifa - Watu wenye umri wa miezi 6 au zaidi ambao watakuwa wakisafiri nje ya nchi wanapaswa kulindwa dhidi ya surua.

Je, nani yuko hatarini mwa kuambukizwa surua?

Mtu yeyote ambaye hajapata chanjo au hajawahi kuwa na surua hapo awali yuko hatarini. Watoto wachanga walio na umri wa chini ya miezi 12 wako hatarini kwa sababu ni wachanga sana kwa hiyo hawajachanjwa.

Je, ninaweza kumlinda vipi mtoto wangu aliye na umri wa chini ya miezi 12?

Ikiwa wazazi au walezi hawajapata chanjo ya MMR au hawakuwa na surua hapo awali, wanapaswa kupata chanjo. Ni muhimu kuhakikisha kuwa watu walio karibu na mtoto wako mchanga hawamwambukizi mtoto wako ugonjwa wa surua na magonjwa mengine (kama vile kifaduro).

Je, itakuwaje iwapo mtu katika familia yangu ana surua au alikaribiana na mtu aliye na surua?

Pigia simu daktari wako, muuguzi au kliniki haraka. Kabla ya kwenda katika ofisi ya mhudumu wa afya, wapigie simu ili uwaambie kwamba huenda wewe au mwanafamilia wako ana surua. Kaa mbali na watu wengine hadi angalau siku nne baada ya vipele kuanza kutokea au kipimo kikithibitisha kwamba huna surua.

Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Surua

Je, wanawake wajawazito wanapaswa kupata chanjo ya surua (MMR)?

Wanawake wajawazito hawapaswi kupata chanjo ya MMR. Wanawake wajawazito wanaohitaji chanjo wanapaswa kusubiri hadi watakapojifungua. Watu wanapaswa kuepuka kupata mimba kwa wiki nne baada ya kupata chanjo ya MMR.

Je, chanjo ya surua ni salama?

Utafiti umeonyesha kuwa chanjo ya surua (MMR) ni salama na fanisi sana. Kupata chanjo ni salama zaidi kuliko kupata magonjwa yoyote ambayo chanjo hulinda dhidi yake.

Je, chanjo hii ina athari zitokanazo na matibabu?

Kama dawa yoyote, chanjo ya surua (MMR) inaweza kusababisha athari zitokanazo na matibabu, athari hizi si sugu:

- Maumivu ulipodungwa sindano
- Homa
- Vipele vidogo
- Tezi zilizovimba kwenye shavu au shingo

Je, chanjo ya MMR husababisha ugonjwa wa tawahudi?

Chanjo hazisababishi ugonjwa wa tawahudi. Kwa hakika, tafiti zimeonyesha kwamba hakuna uhusiano kati ya kupokea chanjo na ugonjwa wa tawahudi. Wanasayansi wamechunguza kwa makini sindano ya MMR na hakuna tafiti zilizopata uhusiano kati ya tawahudi na sindano ya MMR.

Je, ninahitaji chanjo ya nyongeza?

Ikiwa umepata dozi mbili za chanjo ya MMR, huhitaji nyongeza. Ikiwa huna uhakika ikiwa ulichanjwa, zungumza na mtoa huduma wako wa afya.

Je, ninaweza kupata wapi chanjo ya surua?

Mtoa huduma wako wa afya

Columbus Public Health
(614) 645-8180

Franklin County Public Health
(614) 525-3719

Heart of Ohio Family Health Centers
(614) 235-5555

Lower Lights Christian Health Center
(614) 274-1455

Lutheran Social Services (Faith Mission Health Center)
(614) 224-6617

Nationwide Children's Hospital Primary Care Centers
(614) 722-6200

PrimaryOne Health Centers
(614) 645-5500

Southeast Healthcare Services
(614) 225-0990

Duka la dawa au kliniki ya huduma ya karibu
(k.m. Walmart, CVS, n.k.)

Je, ninaweza kupata wapi taarifa zaidi kuhusu surua?

Columbus Public Health
columbus.gov/measles

Franklin County Public Health
myfcph.org/measles

Ohio Department of Health
odh.ohio.gov/know-our-programs/Vaccine-Preventable-Diseases/resources/Measles

Centers for Disease Control and Prevention
cdc.gov/measles

Ilisasishwa 11/2022

THE CITY OF COLUMBUS
ANDREW J. GINTHER, MAYOR
COLUMBUS PUBLIC HEALTH

Franklin County Public Health